

# HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

Mkoa Kilimanjaro

Tel : 27-2756441

Fax : 27- 2756102



OfisiyaMkurugenziMtendaji

S.L.P. 27,

HAI

Tarehe: 8/1/2019

KWA WANANCHI WOTE:

## TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI ZA UWAKALA WA KUKUSANYA USHURU WA MADINI YA UJENZI

ZABUNI NO. LGA/047/2018/2019/HQ/NC/01


1. Halmashauri ya Wilaya ya Hai inakusudia kuweka wakala wa kukusanya mapato mbalimbali ya Halmashauri kwa kipindi cha miezi mitano kuanzia February hadi June 2019.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Hai inapenda kuwaalika watu binafsi, Ushirika, Makampuni, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hii kutuma maombi yao kwa zabuni ifuatayo:

Na.	Aina ya Ushuru	Eneo la Makusanyo
1	Uwakala wa kukusanya Ushuru wa Madini ya Ujenzi, zabuni No. LGA/ 047/ 2018/ 2019/ HQ/NC/01	Eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Hai

3. Mwombaji anapaswa kuwasilisha ombi lake akiambatanisha stakabadhi ya Malipo ya Tshs. 50,000/= kama ada ya maombi, ambayo haitarudishwa (non- refundable fee).
4. Kitabu cha zabuni (Bidding Document) kinapatikana kwenye ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai siku za kazi baada ya

kuonyesha stakabadhi ya malipo. Masharti ya zabuni yanapatikana katika kitabu cha zabuni.

5. Katika barua ya maombi ni lazima Mwombaji aambatanishe maoteo na mchanganuo wa kiasi ambacho mwombaji atawasilisha kwa Halmashauri.
6. Zabuni ziwe katika nakala tatu, nakala halisi moja na nakala nyingine mbili, zifungwe vizuri katika bahasha ya A4 kwa lakiri (wax) na kuandikwa aina ya zabuni, namba ya zabuni, kila bahasha iwe katika bahasha yake na zote ziwekwe katika bahasha moja na maombi yatumwe kwa Katibu, Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Hai, S.L.P 27, HAI
7. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (e-mail) hazitapokelewa.
8. Mwisho wa kutuma maombi ni siku ya Jumanne, Tarehe 22/01/2019, saa 4.00 Asubuhi, na ufunguzi utafanyika hadharani katika Ukumbi wa Halmashauri mara tu baada kufunga kupokea zabuni.
9. Kwa kutokuelewa kipengele chochote unaombwa kufika Ofisi ya Ugavi na Ununuzi kwa ufafanuzi.
10. Halmashauri Wilaya ya Hai haitalazimika kumkubali wakala/ mwombaji yeyote aidha ameomba kwa kiwango cha juu au cha chini.



Yohana E. Sintoo

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**HAI**

**MKURUSENZI MTENDAJI (W)**  
**HAI**